

HALMASHAURI YA WILAYA YA TANGANYIKA

Simu/Nukushi Na.025-2955264
Baruapepe:ded@tanganyikadc.go.tz
Tovuti: www.tanganyikadc.go.tz



S. L. P 01,
MPANDA.
09.09.2022

TANGAZO LA ZABUNI

UTENGENEZAJI WA SAMANI ZA OFISI.

1. Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika imetenga fedha kwa ajili ya kutengeneza samani za ofisi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.
2. Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika inawaalika wazabuni ikiwa ni pamoja na watu binafsi, kampuni, vikundi maalumu, mashirika na taasisi zenye nia na uwezo wa kutengeneza samani za ofisi kwa kuzingatia vigezo vya serikali vilivyoainishwa katika kazi za fundi kama ifuatavyo;

| NA | ZABUNI | NAMBA YA ZABUNI |
|----|--|------------------------------|
| 1 | Utengenezaji wa samani za ofisi kwa ajili ya ofisi ya Mwenyekiti wa Halmashauri na Mkurugenzi Mtendaji | TDC/W/FT/OFC/HQ/2022/2023/01 |
| 2 | Utengenezaji wa samani za ofisi kwa ajili ya ofisi za wakuu wa idara na vitengo | TDC/W/FT/OFC/HQ/2022/2023/02 |
| 3 | Utengenezaji wa samani za ofisi kwa ajili ya ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Wilaya Tanganyika | TDC/W/FT/OFC/HQ/2022/2023/03 |

3. Njia ya ushindani itatumika kumpata mzabuni wa kazi hii bila upendeleo wowote kama ilivyoainishwa katika sheria ya manunuzi ya umma GN No. 446 ya mwaka 2013.
4. Waombaji wote wanakaribishwa kukagua na kujipatia nyaraka za zabuni ambazo zinapatikana ofisi ya katibu wa bodi ya zabuni Halmashauri ya Wilaya Tanganyika S.L.P 01 Mpanda kuanzia saa 01:30 asubuhi hadi saa 09:30 alasiri, kuanzia tarehe 09/09/2022 hadi tarehe 19/9/2022. Jumatatu hadi Ijumaa.


5. Kila mwombaji anapaswa kulipia kiasi cha shilingi elfu ishirini tu (20,000.00) ambayo haitarejeshwa. Malipo hayo yatafanywa kupitia “control number” itakayotolewa na ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika.
6. Sifa za jumla kwa waombaji wa zabuni ni kama ifuatavyo: -
- ✓ Mwombaji ajaze vyema nyaraka zote na kusaini kila kurasa na kuandika juu ya bahasha namba ya zabuni husika.
 - ✓ Mwombaji aambatanishe leseni halali ya biashara, TIN namba, kitambulisho au namba ya Nida
 - ✓ Mwombaji awe na uzoefu usiopungua miaka 3 au zaidi katika kutengeneza samani za ofisi serikalini
 - ✓ Mwombaji aambatanishe cheti cha ukamilifu wa kazi na namba za simu za mwajiri wa awali;
 - ✓ Waombaji wanaweza kuwasilisha mfano wa samani husika siku ya ufunguzi.
7. Maombi yote yafungwe vizuri kwenye bahasha, pamoja na kuandikwa juu ya bahasha maombi husika na kutumwa kwa Katibu wa bodi ya zabuni kwa anuani ifuatayo:-

KATIBU WA BODI YA ZABUNI

S.L.P 1

Tanganyika.

8. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 19/9/2022 siku ya Jumatatu saa 4:00 asubuhi na baada ya hapo maombi hayo yatafunguliwa mbele ya waombaji/wawakilishi wa waombaji katika ofisi ya Katibu wa Zabuni Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika saa 4:00 asubuhi.



Betuely Ruhega

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA TANGANYIKA**

**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
MPANDA**